

MAFUNZO KUHUSU SHERIA YA BARABARA YA MWAKA 2007 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2009 INAYOHUSU MATUMIZI SAHIHI YA HIFADHI YA BARABARA KATIKA WILAYA YA UBUNGO JIJINI DAR ES SALAAM



Na Mwandishi wetu


Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila amesema, sababu ya uwepo wa hifadhi kubwa ya barabara ya Morogoro (Morogoro road) inatokana na umuhimu wa barabara hiyo kwa uchumi wa nchi

Mhandisi Mativila ameyasema hayo jumatano wiki hii, katika mafunzo kwa Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo, kuhusu Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009 inayohusu matumizi sahihi ya barabara, Mafunzo hayo yaliandaliwa na TANROADS na kufanyika wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam.



Alisema kumekuwepo na sintofahamu juu ya matumizi ya hifadhi ya barabara, matumizi ya ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo hususan barabara ya Morogoro ambayo upana wake umekuwa tofauti na maeneo mengine.

Wakitoa maoni yao wakati wa mafunzo hayo, viongozi hao wa wilaya ya Ubungo na wadau wameishukuru TANROADS kwa mafunzo hayo juu ya umuhimu wa hifadhi ya barabara kwani wamesema itawasaidia sana kuwaelimisha wananchi wao na kupunguza baadhi ya malalamiko



'Tumekutana na viongozi kuanzia ngazi ya Kata hadi Wilaya na kuwapa mafunzo, lengo ni kuwa wao wapeleke elimu hii kwa wananchi ili waelewe na kuondoa malalamiko yao' Alisema.

Wakitoa maoni yao wakati wa mafunzo hayo, viongozi hao wa wilaya ya Ubungo na wadau wameishukuru TANROADS kwa mafunzo hayo juu ya umuhimu wa hifadhi ya barabara kwani wamesema itawasaidia sana kuwaelimisha wananchi wao na kupunguza baadhi ya malalamiko

Aidha, viongozi hao na wadau walisisitiza umuhimu wa TANROADS kuendelea kutoa elimu katika maeneo mengine nchini ili kukuza uelewa huo.

Kwa upande wake, Wakili wa Serikali Mwandamizi kutoka TANROADS, Usaje Mwambene akiwasilisha mafunzo hayo alisema, Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 na Kanuni zake za 2009 imeipa mamlaka Wakala ya Barabara Nchini (TANROADS) kuondoa shughuli zote zilizopo ndani ya hifadhi ya barabara.

Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuelimisha, na kuelekeza namna ya kusimamia, kutunza na kufuata sheria ya barabara na kanuni zake kuhusu matumizi sahihi ya hifadhi ya barabara.

